# BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 23 Novemba, 2022.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. **TAARIFA YA SPIKA:**

II. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 01 Novemba, 2022.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Nam. 9 ya 2006 na Kuweka Masharti Yanayohusiana na Watu Wenye Ulemavu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Nam. 9 ya 2006 na Kuweka Masharti Yanayohusiana na Watu Wenye Ulemavu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**MASWALI:**

**<u>Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:</u>**

60. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo Kojani) - Atamuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Pamoja na juhudi kubwa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujali usalama wa wananchi wa jimbo la Kojani kwa kuwajengea kituo kidogo cha Polisi kilichopo katika eneo la Mchangamdogo, kituo hicho hakina usafiri wa aina yoyote, kwa maana ya gari au pikipiki, jambo ambalo haliakisi utendaji wa jeshi hilo katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

(a) Je, ni lini Serikali zetu kwa maana ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), zitapeleka usafiri katika kituo cha Polisi cha Mchangamdogo.

(b) Kwa kuwa kisiwa cha Kojani kina wakaazi wengi wanaohitaji huduma ya ulinzi na usalama kwa kiasi kikubwa. Je, ni lini Serikali itaweka boti japo dogo ya 'fiber' kwa jeshi la Polisi, ili jeshi hilo liweze kuwafikia kirahisi wananchi wa kisiwa hicho.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

71. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana katika mwaka 2021-2022 inadai jumla ya Tsh. 276,048,900 kwa wapangaji 351 wa nyumba za Wakfu na Tsh.48,063,000 kwa wapangaji 56 wa nyumba za Amana.

(a) Je, mpaka sasa zimelipwa kiasi gani.

(b) Je, nyumba hizo ziko ngapi kwa upande wa Unguja na ngapi kwa upande wa Pemba.

117. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kuwa suala la ushahidi Mahakamani ni suala la hiari, kumekuwa na changamoto ya kukosekana kwa mashahidi wanaofika Mahakamani na kutoa ushahidi wakati kesi ikiwa inaendelea mahakamani hapo.

(a) Je, Wizara ina mpango gani katika kulisimamia na kulirasimisha suala la ushahidi Mahakamani.

(b) Je, Wizara ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutoa ushahidi Mahakamani.

(c) Je, ni lini sheria itambana shahidi kutoa ushahidi mahakamani, hususani mzazi au mlezi wa mtoto ambae aliefanyiwa udhalilishaji.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

72. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:sa

Baraza la Mji Kaskazini 'B' lina kawaida ya kutoa Tshs. 10,000,000/- kwa kila Diwani kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maendeleo katika wadi zao. Jambo hili ni zuri na tunalipongeza Baraza la Mji Kaskazini 'B' kwa kuliendeleza jambo hili.

Je, Wizara inatowa wito gani kwa mabaraza mengine na manispaa katika kuiga jambo hili.

## Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

85. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni ukweli usiofichika kuwa, nchini Zanzibar kuna vipaji vingi sana katika michezo tofauti lakini wana michezo wengi hawafaidiki kupitia vipaji vyao.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wana michezo hao, ili wafaidike kimaisha kupitia vipaji vyao.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

35. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili

na Mifugo:

Katika miaka ya nyuma, uchumi wa Zanzibar ulitegemea zao la nazi ambalo lilikuwa kutokana na uzalishaji mkubwa wa minazi ya asili iliyopandwa muda mrefu hapa nchini kwetu. Pamoja na hali hiyo, hivi sasa uzalishaji wa nazi umepungua sana hapa nchini kwa sababu tofauti, ikiwa ni pamoja na sababu ya kuikata minazi ya asili na kuipanda minazi ya kisasa ambayo uzalishaji wake baadae umegundulika kukosa tija.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha minazi ya asili inaendelea kuoteshwa ili isiweze kupotea nchini.

(b) Je, kuna utafiti wowote uliowahi kufanywa na kuonesha ni jinsi gani minazi hiyo ya asili imepotea hadi sasa.

(c) Kwa nini hadi leo hii Serikali haijatangaza kuzuwia ukataji wa minazi hiyo ya asili.

120. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Upatikanaji wa miche kwa wakulima ni jambo muhimu sana. Katika kufikia hatua hiyo, Wizara ya Kilimo ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa, inazalisha miche yenye ubora kupitia vitalu vyake mbali mbali.

Je, miche hii inayotolewa na Wizara kupitia vitalu vyake, inafanyiwa majaribio na kuonekana tija yake kabla haijagawiwa kwa wananchi wetu kwa ajili ya kupandwa.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

23. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wananchi wa Shehia ya Tumbe Mashariki wanaishukuru sana Serikali yao kwa kuwapatia huduma muhimu ya umeme katika soko la samaki lililopo bandarini pamoja na kijiji cha Maafa. Hata hivyo, kuna changamoto ya kutokulipwa fidia kwa waathirika wa maeneo iliyopita miundombinu hiyo.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kutokulipwa fidia kwa wananchi hawa.

(b) Kwa kuwa kulipwa fidia ni haki yao, Je, Wizara yako inawaambia nini wananchi hawa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

1. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Nane kwa juhudi kubwa inazozichukuwa katika kuwawajibisha Wakandarasi Wazawa na Wageni kutokana na kukwamisha au kuchelewesha miradi mbali mbali ya ujenzi inayowalenga wananchi wa Zanzibar.

(a) Je, Serikali inatumia utaratibu gani wa kisheria na kikanuni katika kuwawajibisha Wakandarasi Wazawa na Wageni wanaochelewesha au kukwamisha miradi mbali mbali ya ujenzi hapa nchini.

(b) Je, tokea kuanza kazi kwa Serikali yetu ya Awamu hii ya Nane, ni Wakandarasi wangapi Wazawa na Wageni iliyowawajibisha baada ya kuthibitika kuchelewesha au kukwamisha miradi hiyo.

**Wizara ya Afya:**

65. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hivi karibuni kumekuwa na taarifa kupitia vyombo vya habari mbali mbali pamoja na mitandao ya kijamii kwamba, nchi ya Uganda imekumbwa na janga la gonjwa hatari la EBOLA ambapo watu kadhaa wameathirika na wengine kufariki dunia. Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya nchi za Afrika Mashariki na kwa kuwa Wazanzibari wengi huitumia nchi ya Uganda kupitisha biashara pamoja na kupata elimu katika vyuo mbali mbali vya nchi hiyo.

(a) Ni hatua gani za dharura zilizochukuliwa na Serikali katika kujikinga na ugonjwa huo.

(b) Ni Wazanzibari wangapi walioko Uganda kwa ajili ya shughuli za kikazi pamoja na masomo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

115. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa mtaala wa elimu umeingiza somo la 'Information and Communications Technology (ICT)' kwa elimu ya msingi.

(a) Je, ni yepi malengo ya Wizara ya kuanzisha somo hili kwa elimu ya msingi.

(b) Ni kwa nini hakuna muendelezo wa somo hili kwa upande wa Sekondari, kuanzia Kidatu cha Kwanza hadi cha Nne (Form I to Form IV).

(c) Je, ni manufaa gani mwanafunzi anatarajiwa kuyapata baada ya kumaliza elimu ya lazima (Form IV) kupitia mtaala wa somo hili la ICT.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

50. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kuna tafiti ngapi zilizofanyika katika masuala mbali mbali ya mambo ya kale hivi karibuni na kuleta matokeo chanya.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

39. MHESHIMIWA HABIB ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa kuwa umepita muda mrefu kiwanda cha Makonyo hakikufanya kazi kutokana na uchakavu wa mitambo.

Je, mafuta ya mimea ikiwa ni pamoja na mafuta ya Makonyo, Mchaichai na Mkaratusi, yamezalishwa kwa kilo na tani ngapi kwa mwaka 2021/2022.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

129. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali iliyopo madarakani ya Mhe. Dkt Hussein Ali Mwinyi imeanzisha Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na kwa hatua ya mwanzo imewapatia wavuvi maboti. Tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Nane, lakini kuna tatizo la uharibifu wa kuyang'oa matumbawe hasa kwa watu wanaojihusisha na uvuvi wa juya (nyavu ndogo).

(a) Je, wavuvi wa juya watachukuliwa hatua gani za kisheria kwa uharibifu wa matumbawe.

(b) Je, ni adhabu gani hutolewa kwa wanaopatikana na kosa hilo.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

82. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kuna uvamizi wa kiwanja cha Maendeleo ya Jamii, Shehia ya Chukwani upande wa Buyu.

(a) Je, Serikali inalifahamu suala hilo.

(b) Je, kuna mkakati gani wa kutatua changamoto hiyo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Nam. 9 ya 2006 na Kuweka Masharti Yanayohusiana na Watu Wenye Ulemavu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Zanzibar,**
**23 Novemba, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**